**KISWAHILI**

**KIS 01**

**26/07/2021 2.00 PM – 5.00 PM**

NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

# MTIHANI WA TAIFA KWA SHULE ZA UALIMU, 2020-2021

## SOMO: KISWAHILI

**MCHEPUO:** LANGUAGE-EDUCATION **(LE)**

**MUDA :** **MASAA MATATU**

**MAELEZO:**

1. Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
2. Andika majina yako na nambari yako ya usajili kwenye karatasi ya majibu kama ilivyo kwenye fomu ya usajili.
3. Mtihani huu una sehemu ya I, II, III na ya IV.
4. Jibu maswali yote

   **Sehemu ya I: UFAHAMU** **(alama 30)**

   **Sehemu ya II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** **(alama 30)**

   **Sehemu ya III: FASIHI** **(alama 25)**

   **Sehemu ya IV: UTUNGAJI** **(alama 15)**

5. Andika vizuri nambari ya kila swali.
6. Mwandiko wako usomeke vizuri.
7. Tumia kalamu ya bluu.

**SEHEMU YA I: UFAHAMU (Alama 30)**

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali ya ufahamu

**NDOA YA DADA YANGU.**

Ilikuwa Jumamosi tarehe 15 mwezi wa Juni wakati nilipohudhulia harusi ya dada yangu Mukeshimana Roza aliyefunga pingu za maisha na Kalisa Joni. Harusi yenyewe ilikuwa ya kufana sana. Kabla ya wiki mbili harusi kufanyika familia mbili zilikuwa katika pilikapilika za hapa na pale ili kuandaa sherehe hii ya harusi. Kwa upande wa familia yangu sisi watoto tulikuwa tukitumwa huku na kule kwa kuwaalika watu watakaohudhulia harusi hii. Wazazi wangu waliwaalika wazee majirani na dada yangu akawaalika wenzake hasa wa rika yake. Wote walikuwa wakipelekewa barua za mwaliko. Siku moja kabla, nyumbani kwetu tulifanya usafi na majirani walikuja kumsaidia baba kutayarisha pombe ya mtama, ya ndizi na juisi. Wengine walikuwa wakipamba uga na kujenga nyumba za mahema. Uga wenyewe ulikuwa wa kupendeza sana. Siku hiyo ilipowadia watu walimiminika kuelekea nyumbani kwetu. Asubuhi majira ya saa nne hivi, familia ya bwana harusi ilifika kwetu na kukaribishwa kwa taadhima. Walikuwa wamekuja kuposa na kutoa mahari. Waliandaliwa vyakula na vinywaji mezani wakafurahi sana. Furaha yao ilipandishwa na nyimbo pamoja na ngoma za wachezaji waliokuwa hapo.

Baada ya hapo, Bi harusi alivishwa kanzu nzuri nyeupe na veli. Bwana harusi alirudi kumchukua akiwa na gari la kifahari. Alimkabidhi shada la maua sote tukawapigia makofi, kisha wakaenda kanisani ili kuvishana pete mbele ya Mungu. Nasi tuliandamana nao tukiwa katika magari kadhaa. Watu walipoona mlolongo wa magari hayo waliduwaa wakidhani kuwa kulikuwa na kongamano la kimataifa katika kijiji chetu. Tulipotoka kanisani, tulifurika bustanini kama ilivyoelezwa kwenye barua za mwaliko walizopewa watu. Watu walikuwa wengi sana na sherehe ilikuwa ya kupendeza sana. Tuliandaliwa vinywaji na vyakula tele tele. Bi harusi na Bwana harusi walipewa zawaidi mbalimbali kama vile mikungu ya ndizi, mifuko ya mchele, chupa za asali iliyokamuliwa kutoka kwa masega ya nyuki, mapambo ya aina aina, nk. Watu wote walifurahi sana na kucheza ngoma na nyimbo za utamaduni.

1. Harusi yake Kalisa Joni ilitokea lini? **(alama 2)**
2. Kalisa Joni alioana na nani? **(alama 1)**
3. Maandalizi ya harusi yalifanyika katika muda gani? **(alama 2)**
4. Mwandishi wa habari hii ni wa rika ipi? **(alama 1)**
5. Ni kazi gani zilizofanyika siku moja kabla ya harusi yenyewe? **(alama 5)**
6. Kwenye siku yenyewe ya harusi, familia yake Kalisa Joni ilifika lini kwa bi harusi ilipokuja kuposa na kutoa mahari? Ilikaribishwaje? **(alama 3)**
7. Nini kilichowafanya wafurahi sana familia ya Kalisa Joni walipokuja kuposa na kutoa mahari? **(alama 3)**
8. Kanzu aliyovishwa Mukeshimana Roza ilikuwa ya rangi gani? Nini kingine alichovishwa Bi harusi kabla ya kwenda kanisani? **(alama 4)**
9. Nini kilichosababisha watu kuwapigia makofi Bwana na Bi harusi? **(alama 3)**
10. Mambo yalikuwaje Kalisa Joni na Mukeshimana Roza walipokuwa wanaelekea kanisani kuvishana pete? **(alama 3)**
11. Taja aina tatu za zawadi walizopewa Kalisa Joni na Mukeshimana Roza siku ya harusi yao. **(alama 3)**

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

12. Tumia maneno yafuatayo kujaza nafasi zilizo wazi katika kifungu cha habari kilicho hapa chini: **uchukuzi, miguu, nyingi, Ongezeko, bidii, usitegemee tunahimizwa, mahitaji, lazima, maisha** **(Alama 10)**

Mtu asipofanya kazi hawezi kuyapata ............. yake ya kila siku. Kazi siyo adhabu kwani binadamu ameumbwa ili afanye kazi; ndiyo maana ana akili, mikono, ............., na viungo, vingine vya mwili. Viungo vyote hivi lazima vifanye kazi ili ............ yawe mazuri. Mtu anahitaji kula, kuvaa na kuishi mahali pazuri. Lakini ili kuyapata mahitaji yote, ni ............. afanye kazi. Hivyo basi, tunalazimika kufanya kazi kwa kuwa kazi ni kitendo cha maendeleo. Maendeleo ya mtu huletwa na kazi. Binadamu hupiga hatua za kwenda mbele kimaendeleo akifanya kazi kwa ........... Bila kufanya kazi, maendeleo ya nchi husimama ama hurudi nyuma. Kazi ni za aina ............. Kuna kazi zinazotolewa na serikali au makampuni fulani na kazi za kujiajiri. Kazi zote hizo ni kama vile kilimo, ufugaji, ujenzi, ............, ulindaji wa usalama, ufanyabiashara na kadhalika. Kazi hizi zote zipo ili kujenga nchi yetu. Hii ni kwa sababu nchi yetu itajengwa na mikono

ya wananchi wake. Siku hizi kuna wale wanaochagua kazi na kupuuza nyingine ati si kazi za heshima. Siku hizi kuna ongezeko la wasomi. ………… hili halilingani na kazi zinazotolewa na serikali yetu au makampuni na mashirika ya kibinafsi. Ndiyo maana ………… sisi wenyewe kujitengenezea kazi za kibinafsi, (kujiajiri). Sote hatuwezi kupata kazi za ofisini. Tuna mikono na akili, tengeneza kazi na …………… wengine kwani « Mtegemea cha nduguye hufa maskini. »

13. Oanisha maneno yaliyo katika safu "A" na maana zake zilizo katika safu "B" **(Alama 10)**

| **Safu A** | **Safu B** |
|---|---|
| 1. Mwenyekiti | 1. Kovu lililoko katikati ya tumbo baada ya uzi wa mshipa kukatwa na kukauka. |
| 2. Maarufu | 2. Shule za watoto wadogo wasiozidi miaka mitano |
| 3. Kunufaika | 3. Kufaidika |
| 4. Shule za chekechea | 4. Matendo ya mtu yanayojirudiarudia au tabia. |
| 5. Mwenendo | 5. Karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo ili kuthibitisha kwamba amemaliza au amefaulu mitihani yake. |
| 6. Shahada | 6. Adabu |
| 7. Kitovu | 7. Enye kujulikana sana kila mahali |
| 8. Wajibu | 8. Jambo linalomlazimu mtu kulitimiza. |
| 9. Mchumba | 9. Mtu aliyechaguliwa na watu kuongoza kama vile chama, mkutano au mdahalo. |
| 10. Nidhamu | 10. Mwanamume aliyepeleka posa au mwanamke aliyepelekewa posa na ikakubaliwa na wazazi |

14. Weka tungo zifuatazo katika hali kanushi **(Alama 5)**

a) Wanafunzi wote wamemaliza jaribio.

b) Ningekuwa na mahari ningeoa .

c) Watoto hawa wanataka kucheza au kuimba.

d) Mkigonga mlango mtafunguliwa.

e) Mtoto amekwenda shuleni.

15. Weka tungo zifuatazo katika usemi wa taarifa. **(Alama 5)**

a) "Futa ubao" mwalimu ananiambia.

b) "Kesho tutakua na wageni kutoka Tanzania" kiongozi aliarifu raia wa kijiji chake.

**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)**

16. Jaza methali zifuatazo: **(Alama 5)**

a) Mvumilivu hula ...........

b) Baada ya dhiki ..........

c) Usipoziba ........... utajenga ukuta

d) Tamaa mbele ........... nyuma.

e) Dalili za mvua ni ..........

17. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yanavyotumiwa katika fasihi: **(Alama 10)**

a) Fasihi andishi

b) Riwaya

c) Tamthilia

d) Mshororo

e) Ubeti

18. Eleza maana ya nahau zifuatazo: **(Alama 10)**

a) Kuaga dunia

b) Kukata tamaa

c) Kuvaa miwani

d) Kujipa moyo.

e) Kula chumvi nyingi.

## SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 15)

19. Tunga insha yenye mada ifuatayo: "Umuhimu wa Kiswahili katika jamii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki." Tumia maneno kati ya 200 na 250.

**(Alama 15)**

**-Mwisho-**

UKURASA TUPU

UKURASA TUPU